Unaweza kupakua toleo la Masharti haya nje ya mtandao hapa.

Maboresho ya mwisho yalikuwa:
Masharti haya yanatumika baina yako na Bolt pindi unapokubali kuweka machapisho katika gari. Unaweza kusitisha makubaliano haya muda wowote kulingana na kifungu namba 5.1.

**1. Ufafanuzi**
Katika mkataba huu, ufafanuzi ufuatao unatumika:
1.1. **Vifaa vya Machapisho** : inamaanisha vibandiko vya kuweka kwenye magari (au vifaa vingine) vitolewavyo na Bolt.
1.2. **Muda wa Machapisho**: muda wa miezi mitatu isipokuwa pale mkataba uatakositishwa mapema kadri ya matakwa ya mkataba huu. haya
1.3. **Chapisho**: Kubandika vifaa vya machapisho/alama kwenye magari teule
1.4. **Bolt**: inamaanisha Bolt Operations OU kampuni binafsi iliyuoundwa na kusajiliwa chini ya sheria za Jamhuri ya Estonia yenye namba za usajili 14532901, usajili wa ofisi- Vana-Lõuna tn 15, Tallinn 10134, Jamhuri ya Estonia
1.5. **Bolt Group**: inamaanisha Bolt na makampuni yake.
1.6. **Masharti ya kawaida ya Bolt**: Masharti na vigezo , sera na miongozo yote itolewayo na Bolt Group mara kwa mara ambayo inatumika kwako kuhusiana na matumizi ya jukwaa na programu ya Bolt Group
1.7. **Eneo/Maeneo Husika** : maeneo kwenye Gari/Magari Husika kwa ajili ya kuonyesha alama/vifaa vya machapisho kama ilivyokubalia kati yako na Bolt.
1.8. **Gari/Magari Husika**: magari yatakayotumika kuonyesha alama/vifaa vya machapisho kama ilivyo ilivyokubaliwa kati yako na Bolt.
1.9. **Motisha**: motisha utakayopata pale utakapo tekeleza wajibu wako katika mkataba huu kama itakavyowasilishwa kwako na Bolt kwa njia ya maandishi mara kwa mara.
1.10. **VAT:** Kodi ya ongezeko la thamani inayotozwa kulingana na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 marudio ya mwaka 2019.

**2. Chapisho**
2.1. Unakubali kubandika, kuonyesha na kuweka vifaa vya machapisho kwenye gari teule kwa kila Muda wa Chapisho kwa mujibu wa masharti ya mkataba huu. Kwa kubadilishana Bolt itakuruhusu kupata Motisha kwa mujibu wa kifungu 2.2.
2.2. Kupata kwako Motisha kutategemea wewe kukamilisha masharti ya ziada uatakayopewa na Bolt kwa njia ya maandishi. . Endapo utashindwa kutekeleza masharti hayo hautakuwa na haki ya kupata Motisha. Tafadhali walisiana na Bolt bila kuchelewa kama unahitaji ufafanuzi juu ya masharti yakayotumika kwako. Endapo haukubaliani na masharti hayo, unaweza kusitisha Mkataba huu muda wowote kwa mujibu wa kifungu namba 5.1.
2.3. Unaweza kuombwa kuchangia kwenye gharama za Chapisho. Pale inapohitajika , utajulishwa gharama hizokabla ya Vifaa vya Machapisho kutolewa. Kwa kukubali kuwekewa machapisho kwenye gari husika, unakubali pia kulipa gharama hizo. Endapo haukubaliani na gharama hizo, usiweke au kuruhusu kuwekwa kwa Chapisho kwenye Gari/Magari Husika.
2.4. Ni lazima uweke kuweka Chapisho Eneo/Maeneo Husika na katika mazingira mazuri muda wote. Ni lazima kutoa taarifa kwa Bolt kama Chapisho litaharibika au litahitajika kubadilishwa.
2.5. Bolt inaweza kukutaka kuthbitisha kwamba unatekeleza wajibu wako katika Mkataba huu. Unakubali kutoa ushahidi kwa Bolt pale utakapotakiwa mara kwa mara ikiwemo ushahidi wa picha kuonyesha Chapisho limewekwa kwenye Gari Husika.
2.6. Hautakuwa na haki ya kupata motisha yoyote baada ya Mkataba huu kufikia ukomo ama

kusitishwa.

**3. Ukomo na Kuhuissha**
3.1. Muda wa Machapisho kwa kipindi cha kwanza utaanza siku ya kwanza ya kuwekwa kwa Chapisho kwenye Gari?magari Husika au siku nyingine yoyote itakayokubaliwa na Bolt.
3.2. Isipokua kwa kusitishwa mapema kwa Mkataba, Mkataba huu utahuishwa moja kwa moja baada ya kuisha kwa Muda wa Chapisho kwa muda wa miezi mitatu mfululizo (kila mmoja ukiwa muda mpya wa machapisho)

**4. Udhamini, Wajibu na Fidia**
4.1. Unaihakikishia Bolt kuwa:
4.1.1. Utadumisha katika kipindi cha mkataba vibali na ridhaa za kuingia na kufuata matakwa ya Mkataba huu, ikiwemo ridhaa ya mwenye gari, bima na mdhibiti wa biashara za matangazo (pale itakapotakiwa).
4.1.2. Kutekeleza wajibu wako katika Mkataba huu hakutavunja mkataba mwingine wowote ulioingia, wala kubatilisha au kuharibu bima ya Gari/Magari Husika.
4.1.3. Utatekeleza wajibu wa kisheria ambao unaweza kutumika kwako kuhusiana na kifungu cha Motisha (ikiwemo wajibu wako wa kulipa kodi)
Na kwa kuingia kwenye mkataba huu, unakubali kutoa fidia kwa Bolt Group itakapotokea hasara, uharibifu, gharama au madai yanayoweza kujitokeza.
4.2. Unashauriwa kuwa uwekaji wa vibandiko vyovyote ikiwemo Chapisho kwenye gari lolote inaweza kusababisha uharibifu wa rangi ya gari hilo na umekubali kufanya uchunguzi wako na kutathmini kama Gari/Magari husika yanaweza kuwekewa Chapisho. Bolt Group haitakubali kuwajibika kwa uharibifu uliosababishwa na kuweka au kutoa Chapisho kwenye gari husika na kwa kuingia kwenye Mkataba huu unakubali kuifidia Bolt Group kutokana na hasara, uharibifu, gharama na madai yanayoweza kujitokeza.

**5. Kusitisha**
5.1. unaweza kusitisha Mkataba huu muda wowote kwa kutoa notisi ya maandishi isiyopungua kipindi cha siku saba (7) kupitia programu ya Bolt.
5.2. Bolt inaweza kusitisha Mkataba huu muda wowote kwa kutoa notisi ya maandishi isiyopungua kipindi cha siku saba (7) (ambayo inaweza kutolewa kwa kupitia barua pepe au programu ya Bolt).
5.3. Bolt inaweza kusitisha Mkataba huu mara moja katika muda wowote pale utakapokuwa umevunja Mkataba huu au Masharti ya Kawaida ya Bolt au umefanya kitu chochote ambacho kwa maoni yaBolt kinaweza kuchafua sifa za Bolt kwa kukupa notisi ya maandishi (ambayo inaweza kutolewa kwa kupitia barua pepe au programu ya Bolt). Katika mazingira haya Bolt itakuwa na haki ya kukataa kutoa Motisha ambayo ungetakiwa kupewa kutokana na Mkataba huu.
5.4. Mkataba huu utasitishwa mara moja pale matumizi yako kwenye jukwaa na programu ya Bolt Group yatakuwa aymezuiwa kwa kulingana na Masharti ya Kawaida ya Bolt. Katika mazingira haya, Bolt itakuwa na haki ya kukataa kutoa motisha ambayo ungetakiwa kupewa kutokana na Mkataba huu.
5.5. Pale ambapo Mkataba huu utasitishwa, Muda wa Machapisho utakuwa umeisha. Utatakiwa kutoa machapisho kwenye Gari/Magari Husika haraka na kuyatupa. Unakubali kulipia gharama yoyote inayohusiana na utoaji wa Chapisho. Pia unakubali kuwa Bolt inaweza kukutaka kuonyesha ushahidi wa picha ya utoaji wa Chapisho kwenye Gari/Magari Husika ambapo utalazimika kutoa pale itakapohitajika.

**6. Vipengele vingine**

6.1. Malipo yoyote utakayopokea kutoka Bolt kutokana na Mkataba yatajumuisha na kodi ya ongezeko la thamani na kodi nyingine zitakazohusiana na malipo hayo isipokuwa kama imekubaliwa tofauti kwa maandishi.

6.2. Unakubali kuwa Bolt inaweza kukukata ada yoyote inayotakiwa kulipwa kutokana na Mkataba huu dhidi ya malipo yoyote unayodai kwa Bolt Group. Pia unakubali kuwa Bolt inaweza kukukata malipo yoyote yanayowezakuwa yamelipwa kwa ziada dhidi ya malipo yoyote unayodai kwa Bolt Group kutokana na Mkataba huu.

6.3. Bolt inaweza kubadilisha namna ya utoaji wa Motisha mara kwa mara pale ili mradi hakutakuwa na athari yoyote kwenye thamani au muda wa utoaji wa Motisha.

6.4. Haki miliki zote kwenye Chapisho zitabaki kwenye umiliki wa Bolt Group na machapisho yote yasinakiliwe, yasisambazwe, yasiwekwe mtandaoni au yasichapishwe kwa njia yoyote bila kupata kwanza ruhusa ya maandishi kutoka Bolt Group.

6.5. Unakubali kuwa kuonyesha Chapisho baada ya Mkataba huu kuisha kutapelekea utumiaji wa haki miliki ya Bolt Group usio sahihi na utatakiwa kulipa fidia kwa Bolt Group kwa gharama zote watakazokuwa wamepata (ikiwepmo gharama za kitaalamu na za kisheria) zinazohusiana na utumiaji huo usio sahihi na utahakikisha unaondoa kupata kwa haraka Chapisho.

6.6. Pale kipengele chochote cha Mkataba huu kitaonekana kutoweza kutekelezeka, wahusika wote katika Mkataba huu wanakubadiliana kuwa watabadilisha kipengele hicho na kuweka kipengele kitakachoweza kutekelezwa kisheia ambacho kitaendana na nia ya kipengele kilichofutwa na Mkataba utatafsiriwa ipasavyo.

6.7. Kushindwa au kuchelewa kutekeleza sharti lolote katika Mkataba huu hakutapelekea msamaha wa sharti hilo.

6.8. Mkataba huu utazingatia sheria, mamlaka ya mahakama zile zile kama ilivyo kwenye Masharti ya Kawaida ya Bolt (kama zitakavyoweza kutumika kwako).

6.9. Bolt inaweza kuboresha masharti ya Mkataba huu mara kwa mara kwa kukupatia notisi ya siku zisizopungua saba (7) inayohusiana na maboresho hayo. Tolea la masharti ambayo yatatumika kwako kwenye muda wa Chapisho yatabaki kama toleo la masharti haya ambayo yalikua kwenye utekelezaji siku ya kwanza ya muda wa Chapisho.

6.10. Kifungu cha 5.5. na 6 kitaendelea hata baada ya Mkataba huu kusitishwa.

6.11. Taarifa binafsi yoyote iliyotumika kwenye Mkataba huu itachakatwa kwa kufuata Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44 pamoja na Kanuni za ukusanyaji na uchakataji wa tarifa binafsi za mwaka 2023 na notisi binafsi ambazo zinapatikana hapa.

**Mwisho wa Mkataba**